



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 17

Agosti 1-31, 2020



1938 - 2020

Buriani Rais Mstaafu, Benjamin William Mkapa

PUMZIKA KWA AMANI

SERIKALI KUFIKISHA UMEME MGODI WA STAMIGOLD SEPTEMBER UK. 2



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

SERIKALI KUFIKISHA UMEME MGODI WA STAMIGOLD SEPTEMBER

**Veronica Simba –
Biharamulo**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ameuagiza uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhakikisha kuwa, ifikapo mwishoni mwa mwezi Septemba, mwaka huu, umeme uwe umefikishwa katika Mgodi wa Dhahabu wa Stamigold uliopo Biharamulo.

Alitoa maelekezo hayo Julai 6, 2020 alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kupeleka katika Mgodi huo unaomilikiwa na Serikali.

Akizungumza na viongozi wa Mgodi huo, Dkt Kalemani alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutenga fedha za kutosha kuweza kutekeleza Mradi huo mkubwa.

“Nataka nitoe taarifa kwenu watu wa Stamigold, kwamba Mheshimiwa Rais ameshatuagiza kutekeleza Mradi huo. Tunazo shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya kuleta umeme hapa.”

Akieleza zaidi, alisema ujenzi wa Mradi huo utakaotumia takribani miezi miwili na nusu, unatekelezwa kwa fedha za ndani kwa asilimia 100.

Aidha, alieleza kuwa umeme utakaopelekwa Mgodini hapo unatolewa eneo la Mpomvu, mkoani Geita, umbali wa takribani kilomita 100 na kwamba ili kuhakikisha umeme huo unakuwa wa uhakika, zitawekwa transfoma mbili katika eneo husika.

Alisema, Serikali imedhamiria uchimbaji wa madini wa aina zote utumie umeme ili uwe na tija hivyo kuwawezesha wachimbaji



Vibarua wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakishirikiana kuvuta nguzo katika kijiji cha Kunankwa, Geita, kilicho jirani na Mgodi wa Dhahabu wa Stamigold. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Julai 6, 2020 kukagua ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme unaotarajiwa kufikishwa katika Mgodi huo, Septemba mwaka huu.

kulipa tozo stahiki na kutoa gawio kwa Serikali.

Waziri aliutaka uongozi wa Stamigold, baada ya kufikishiwa umeme, kuandaa mapendekezo ya mahitaji yao ya baadaye ya umeme ili Serikali kupitia Wizara ya Nishati ijipange kuwapatia huduma hiyo.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi kwa

Waziri, Kaimu Meneja wa Mgodi, Mhandisi Rashid Lulamka, alisema umeme utakapofikishwa Mgodini hapo, utasaidia kuokoa takribani shilingi milioni 700 kwa mwezi ambazo hutumika kununulia mafuta ya kuendesha mitambo.

“Kwa sasa, tunatumia takribani shilingi bilioni

moja kwa mwezi kwa ajili ya kununua mafuta. Tukipata umeme, matarajio yetu ni kushuka kwa kiwango hicho hadi shilingi milioni 300,” alifafanua.

Katika ziara hiyo, Waziri aliambatana na viongozi pamoja na wataalamu mbalimbali kutoka Wizarani, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

TUTAKUKUMBUKA DAIMA MZEE MKAPA

Taifa likiwa lingali na majeraha mabichi ya kuondokewa na Rais Mstaafu wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa, sisi wa Nishati News Bulletin, tunaamini Mzee wetu ataendelea kuishi kati yetu.

Tunaamini hivyo kutokana na kazi kubwa na njema aliyofanya katika nchi yetu na hata nje ya Tanzania, katika kipindi chake cha uongozi lakini pia hata baada ya hapo.

Yako mengi ya kukumbukwa aliyoyatenda Mzee Mkapa na yamekuwa yakielezwa kutoka kila pande ndani na nje ya nchi. Katika hayo mengi, sisi wa Nishati News Bulletin tutamkumbuka zaidi kwa mambo makuu mawili.

La kwanza ni kwa kuanzishwa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini katika kipindi chake cha Uongozi. Hayati Mkapa aliuona umuhimu wa wananchi kupata habari za yale yanayotekelezwa na Serikali yao. Jarida hili ni sehemu tu, tena ndogo, ya matokeo chanya ya uthubutu huo uliofanywa na Mzee wetu.

Wizara ya Nishati, kupitia Kitengo chake cha Mawasiliano Serikalini, hutumia Jarida hili pamoja na mbinu nyingine mbalimbali za mawasiliano, kuwafikishia wananchi taarifa za utekelezaji wa kazi mbalimbali chini ya Wizara kwa lengo la kuwahabarisha lakini pia kuwaelimisha.

Jingine ambalo kwa namna ya pekee sisi wa Nishati News Bulletin tutamkumbuka Mzee Mkapa ni uhamasishaji wake wa 'Ukweli na Uwazi' katika kutekeleza majukumu yetu.

Hamasa hiyo siku zote imekuwa chachu kwetu kuwahabarisha wananchi pasipo kificho, kile ambacho Serikali, kupitia Wizara yetu inafanya ili kuwajengea uelewa mpana wa Sekta ya Nishati.

Kwa hayo na mengine mengi aliyofanya Hayati Mkapa, yanatupa ujasiri wa kuamini kuwa japokuwa ametuacha kimwili, lakini ataendelea kuishi kati yetu maana kazi zake zilizotukuka zinaendelea kutunufaisha.

Buriani Mzee Mkapa. Kwetu sisi daima utaishi.



BODI YA UHARIRI

Mhariri

Veronica Simba
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

Waandishi

Veronica Simba
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mtumba Dodoma, S.L.P.
2494, 40474 Dodoma

www.nishati.go.tz

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara_ya_nishati_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)

Katunika Ki-nishati

WIZARA YA NISHATI INAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUOMBOLEZA KIFO CHA RAIS MSTAAFU, HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA. DAIMA TUTAKUENZI. PUMZIKA KWA AMANI MZEE WA UWAZI NA UKWELI.

HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA 1938-2020

TUNATOA POLE KWA MHESHIMIWA RAIS DKT. JOHN POMBE MAGUFULI, MAMA ANNA MKAPA NA WANAFAMILIA PAMOJA NA WATANZANIA WOTE.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemami (wa pili kutoka kulia), akiwa katika ziara ya kazi Julai 6, 2020, kukagua ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme unaotarajiwa kufikishwa katika Mgodu wa Dhahabu wa Stamigold, uliopo Biharamulo, Septemba mwaka huu.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemami (mwenye miwani - mbele) na Ujumbe wake, akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Mgodu wa Dhahabu wa Stamigold. Waziri alitembelea Mgodu huo Julai 6, 2020 kukagua ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme unaotarajiwa kufikishwa katika Mgodu huo, Septemba mwaka huu.

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemami (katikati) akielekeza jambo kwa uongozi wa Mgodu wa Dhahabu wa Stamigold, alipitembelea Mgodu huo kukagua ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme, Julai 6 mwaka huu.



Sehemu ya Mgodu wa Dhahabu wa Stamigold. Taswira hii ilichukuliwa Julai 6, 2020 wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemami (hayupo pichani), kukagua ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme unaotarajiwa kufikishwa katika Mgodu huo, Septemba mwaka huu.



Rais Magufuli azungumzia umeme vijijini

Na Teresia Mhagama

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amesema kuwa Serikali imeendelea kusambaza umeme katika vijiji mbalimbali nchini kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Aliyasema hayo Juni 2020, wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (standard gauge) kwa sehemu ya kwanza ya Dar es Salaam - Morogoro.

Alisema kuwa, mwaka 2015 takribani vijiji 2000 vilikuwa na umeme lakini kwa sasa vijiji zaidi ya 9000 vimesambaziwa umeme na kubakiwa na vijiji takribani 3000 ambavyo vinaendelea kusambaziwa umeme.

“Hii si miujiza, ni juhudi na maarifa ambayo tumeamua sisi wote watazania kuisimamia,” alisema Dkt. Magufuli

Kuhusu Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere utakaozalisha megawati 2115, alisema kuwa Bwawa hilo likianza kuzalisha umeme, bei ya nishati hiyo itashuka, viwanda vitapata umeme wa kutosha, vijana wataendelea kupata ajira na uchumi wa Tanzania utazidi kukua.

Kuhusu mgawo wa umeme alisema kuwa, kwa miaka mingi kumekuwa na suala la mgawo wa umeme lakini kwa miaka karibu mitano sasa hakuna mgawo wa nishati hiyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabwawa ya umeme kuwa na maji wakati wote ya kuzalisha umeme huo.

Kwa upande wake Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari alizungumzia kuhusu uwepo wa umeme wa uhakika wa kuendesha



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Treni ya kisasa ya mwendokasi, alisema kuwa Treni hiyo itakayokuwa ikitumia megawati 60 za umeme, itaendeshwa kwa kutumia vyanzo mbalimbali hivyo haitasimama.

Alisema kuwa, Treni hiyo itaendeshwa na

umeme kutoka mitambo ya Kinyerezi, Bwawa la Mtera na Kidatu pamoja na umeme kutoka Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa awamu ya kwanza wa miundombinu ya umeme itakayoundesha treni hiyo

kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika.

Vilevile alisema kuwa, Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu hiyo itajengwa kutoka Morogoro -Dodoma-Singida na inatarajiwa kukamilika mwaka 2021.

MGALU AWAONYA WAKANDARASI WANAOSUSUA

Hafsa Omar - Katavi

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema Serikali haitasita kusitisha mkataba wa Mkandarasi yeyote ambaye ataonekana kusuasua katika kutekeleza majukumu yake na kwenda kinyume na mkataba wake wa kazi.

Aliyasema hayo Julai 7, 2020, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kenswa Nsimbo, kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi, kabla ya kuwasha umeme kwenye kijiji hicho.

Maelezo hayo ya Naibu Waziri ni kutokana na kutoridhishwa na kasi ya usambazaji umeme mkoani humo, inayofanywa na Kampuni ya China Railway Construction Electrification Bureau Group Co Ltd (CRCEBG)

Aidha, alisema Serikali tayari imesitisha mkataba



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati), akiwasili kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Kenswa Katumba kilichopo katika Kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, Julai 7, 2020, akiwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme.

wa mkandarasi wa mradi wa Umeme Vijijini (REA) mkoani Mwanza,

kwa sababu hakuweza kutekeleza majukumu yake kama mkataba

unavyoeleza.

“Bado kasi ya mkandarasi haijaturidhisha. Kwa sasa tumeamua kutengua mikataba kwa wakandarasi wasioendana na kasi yetu. Leo tutakaa nao kupitia mpango kazi wao na tutakubaliana kwa mara ya mwisho na mkandarasi huyo, na asipobadilika tutatengua mkataba wake tumpe mwengine,” alisema.

Alifafanua kuwa, wakandarasi wote nchini wanayafahamu vizuri maeneo yao ambayo waliomba kufanyia kazi na kuzifahamu changamoto za maeneo hayo hivyo aliwataka wakandarasi hao kuacha kutoa sababu kuwa miundombinu inawakwamisha kutekeleza kazi zao kwa



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kenswa Katumba kilichopo katika Kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, kabla ya kuwasha umeme kwenye kijiji hicho, Julai 7, 2020.

MGALU AWAONYA WAKANDARASI WANAOSUSUA

INATOKA UK.

6

wakati.

Alieleza kuwa, Serikali haipo tayari kurudishwa nyuma katika juhudi zake za usambazaji umeme nchini, ambapo inatarajiwa ifikapo mwisho wa mwezi wa Julai jumla ya vijiji 10,446 vitakuwa tayari vimesambaziwa umeme hivyo akawataka wakandarasi wote wa miradi ya REA kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha lengo hilo.

Hata hivyo, Mgalu aliwatoa hofu wananchi wa Mkoa huo kuwa vijiji vyao vyote vilivyosalia vitapata umeme kupitia mradi wa REA III Mzunguko wa Pili ambao unatarajiwa kuanza Septemba mwaka huu.

“Naomba kuwahakikishia kuwa Katavi kazi inaendelea na



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (wa pili-kushoto) akikata utepe kuashiria kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya kijiji cha Tambaza Kenswa Nsimbo, Kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, Julai 7, 2020. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Rachel Kasanda.

vijiji vilivyosalia vitaingia kwenye mradi wa REA III Mzunguko wa Pili. Mradi huo utafanya Katavi yote kuwa na umeme kwahiyo naomba mkae mkao wa kupokea mradi huo wa

umeme,” alisema Mgalu.

Aliongeza kuwa, Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya mradi wa ujazilizi, ambao utapeleka umeme kwenye vitongoji

vyote nchini ambapo tayari mkandarasi ameshapatikana na mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Agosti mwaka huu.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kusambaza umeme kwa kasi kubwa kwasababu inafahamu kuwa mahitaji ya huduma hiyo yanaongezeka siku hadi siku na kwa kasi kubwa na kwamba imejipanga kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata huduma hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Rachel Kasanda alisema jumla ya vijiji 44 vimeunganishiwa umeme mkoani humo ambapo idadi hiyo ni ndogo kulinganisha na mahitaji ya watu wengi wanaohitaji huduma, hivyo kumtaka mkandarasi kuongeza kasi ya usambazaji wa huduma hiyo.

Pia, aliishukuru Serikali kwa juhudi zake za kuunganisha Mkoa wa Katavi kwenye gridi ya Taifa hatua ambayo itawezesha kuondokana na mfumo wa kutumia umeme wa mafuta ambao una gharama kubwa kwenye uendeshaji wake ambapo zaidi ya shilingi milioni 21 zinatumiwa kwa siku moja, sawa na shilingi milioni 648 kwa mwezi.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri pia alitembelea kituo cha kupokelea umeme wa gridi ya Taifa kilichopo katika kijiji cha Kampuni na kuwataka wakandarasi wa mradi huo kufanya kazi kwa kasi kubwa ili kumaliza kujenga mradi kwa wakati uliopangwa.

Pia, aliwasha umeme katika Zahanati ya kijiji cha Tambaza Kenswa Nsimbo, Kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda.



Wananchi wa kijiji cha Kenswa Katumba kilichopo katika Kata ya Katumba, Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme kwenye kijiji hicho, Julai 7, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoani wa Katavi, wakikagua ujenzi wa kituo cha kupokelea umeme wa gridi ya Taifa Mpanda, kilichopo katika kijiji cha Kampuni, wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, akiwa katika ziara ya kazi, Julai 7, 2020.

DKT KALEMANI AWACHARUKIA WANAOTOZA BEI KUBWA ZA UMEME

Veronica Simba – Sengerema

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, ametoa onyo kali kwa wazalishaji binafsi wa umeme, wanaowatoza wananchi gharama kubwa tofauti na bei elekezi ya Serikali.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza, Julai 7, 2020, Waziri alisisitiza kuwa gharama stahiki ya umeme kwa wananchi wote wenye matumizi ya kawaida ni shilingi 100 tu kwa uniti moja.

Alisema, wananchi wanapaswa kutozwa gharama inayofanana katika maeneo yote nchini kwani wote wana haki



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme, Julai 7, 2020.

sawa. “Bei hiyo ni kwa maeneo yote nchini vikiwemo visiwa na ni kwa umeme wa aina zote pasipo kujali ni wa TANESCO au kutoka

kwa wazalishaji binafsi wanaotumia umeme jua na aina nyinginezo,” alisisitiza Waziri.

Alitoa agizo kwa viongozi wa Serikali,

hususian Wakuu wa Wilaya kote nchini, kuwachukulia

INAENDELEA UK. 10



Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, akizungumza wakati wa Mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto) na wananchi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza (hawapo pichani) Julai 7, 2020. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme.



Mzee Julius Luzendaze, akitoa maoni yake kuhusu upatikanaji wa umeme, wakati wa Mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) na wakazi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza, Julai 7, 2020.

DKT KALEMANI AWACHARUKIA WANAOTOZA BEI KUBWA ZA UMEME

INATOKA UK.

9

hatua wazalishaji binafsi wa umeme, watakaobainika kukiuka mwongozo huo wa Serikali.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali, hususani wanaoishi visiwani, kwamba wamekuwa wakitozwa gharama kubwa na wawekezaji binafsi wa umeme hali inayosababisha wengi wajisikie kama wakimbizi ndani ya nchi yao.

Waziri alisema kamwe Serikali haitavumilia tabia za aina hiyo zinazooneshwa na baadhi ya wawekezaji binafsi wa umeme kwani imewaamini kutenda haki katika kuwafikishia umeme wananchi hao ambao hawajafikiwa na gridi ya Taifa.

Hata hivyo, alibainisha kuwa Serikali inaendelea na zoezi la kupeleka umeme wa gridi ya Taifa katika visiwa vyote nchini kwa



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemmani (kulia), akieleza dhamira ya ziara yake kwa Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole (kushoto), alipowasili wilayani humo Julai 7, 2020 kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme.

kupitisha nyaya chini ya maji yanayozunguka visiwa hivyo.

Aliwataka wananchi wa visiwani ambao hawajafikiwa na huduma hiyo kuwa watulivu kwani huduma hiyo itawafikia wote awamu kwa awamu.

Akiwa katika Mkutano huo, Waziri aliagiza

kukamatwa na kuhojiwa wawakilishi wa kampuni ya kuzalisha umeme wa jua iitwayo Jumeme, baada ya wananchi wa kisiwa cha Maisome wilayani humo, kuwatuhumu kuwa wamekuwa wakiwauzia umeme kwa gharama ya shilingi 3,500 kwa uniti moja.

Akizungumza katika

Mkutano huo wa Waziri, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, alipongeza hatua za makusudi ambazo Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imekuwa ikizichukua katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya umeme.

Aidha, alitoa shukrani na pongezi kwa Serikali, kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, kutokana na kutatuliwa kwa changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara, iliyokuwa ikiwakosesha amani wananchi hao.

“Umeme sasa haukatiki tena mara kwa mara kama ilivyokuwa awali na hata inapotokea, TANESCO wanatoa taarifa kwa wakati wakieleza sababu za kukata, muda utakaotumika kurejesha huduma hiyo pamoja na maeneo yatakayoathirika,” alisema.

Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme wilayani humo.



Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Dauson Kamaka (kulia) na Msimamizi wa Miradi ya Umeme Vijijini, Kanda ya Ziwa, Mhandisi Ernest Makale (kushoto), wakifuatilia Mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemmani (hayupo pichani) na wakazi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza (hawapo pichani). Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme, Julai 7, 2020.



Sehemu ya umati wa wakazi wa kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema, Mkoa wa Mwanza, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemmani (hayupo pichani), alipofanya ziara wilayani humo Julai 7, 2020 kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme.

Kampuni ya NAMIS yanyooshewa kidole kusuasua mradi wa PERI URBAN

Zuena Msuya - Pwani

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ameionyooshea kidole Kampuni ya ukandarasi ya Namis inayotekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji (Peri Urban), Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, na Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, kwa kusuasua kutekeleza mradi huo na kuiagiza kuongeza kasi hadi kufikia mwishoni mwa Agosti, 2020 iwe imekamilisha kazi ya utekelezaji wa mradi huo.

Mhandisi Masanja alisema hayo Julai 11, 2020 wilayani Kisarawe mkoani Pwani wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaotekelezwa kwa kasi isiyoridhisha, ikilinganishwa na makubaliano na matakwa ya mkataba husika, huku mkandarasi akieleza sababu zinazochangia kusuasua kwa mradi huo.

Mhandisi Masanja alieleza kuwa, kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 39 ambayo ni tathmini ya chini na makubaliano ya mkataba yanayoelekeza kuwa tangu kusainiwa kwa mkataba huo na kuanza kwa utekelezaji wa mradi mwezi Desemba, 2019, hadi kufikia sasa mradi huo ulitakiwa kuwa umekamilika kwa asilimia 77.

Alimtaka mkandarasi huyo kuongeza nguvu kazi na magenge ya watu watakaofanya kazi usiku na mchana ili kwenda sambamba na kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike ndani ya muda uliopangwa.

Vilevile alimshauri mkandarasi huyo kununua vifaa vya kutekeleza mradi kama nguzo, nyaya, mita za LUKU na vifaa vingine vinavyohitajika katika ujenzi wa mradi huo kutoka kwa wazalishaji wenye uwezo wa kuzalisha vifaa hivyo ili kurahisisha na kukamilisha haraka utekelezaji wa mradi huo.

“Kasi hii hairidhishi



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akichora ramani chini ikiwa ni kutoa maelekezo kwa wasimamizi na mkandarasi anayetekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji (Peri Urban), alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo Wilaya ya kisarawe, mkoani Pwani, Julai 11, 2020.



Moja ya nyumba zilizopo katika maeneo yanayopitiwa na mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji (Peri Urban), Kijijini Vilabwa, ikiwa tayari imetandaziwa nyaya tayari kwa kuunganishwa umeme. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, Julai 11, 2020.

kabisa. Utekelezaji wa mradi unasuasua. Hizi sababu unazoeleza kuwa zimechangia kukucheleweshwa wala sizikubali kwa kuwa kuna wakandarasi wenzako mmeanza kazi pamoja na wote mmelipwa fedha sawa, wenzako wamepiga hatua mbele na watalimiza kwa wakati, wewe ni nini kinakukwamisha?” alihoji.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu, kampuni ya NAMIS ilipewa jukumu la kusambaza umeme katika vijiji 62 vya Peri Urban. Kati ya hivyo, vijiji 32 viko

Kampuni ya NAMIS yanyooshewa kidole kusuasua mradi wa PERI URBAN

INATOKA UK.

11

maeneo ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam na vijiji 30 viko maeneo ya Kisarawe. Kazi ya utekezaji wa mradi huo inaendelea lakini kwa kasi isiyoridhisha.

“Mkandarasi ameahidi na tumekubaliana kuwa hadi kufikia Julai 15, 2020 nguzo zote zilizosimikwa ziwe zimevutwa nyaya katika maeneo yote ya mradi, na kwamba ataendelea kuchimbia nguzo na kuvuta waya katika maeneo mengine ambayo bado hayajafikiwa. Sambamba na hilo, ataunga wateja katika maeneo hayo, na mimi nitakuja tena mwishoni mwa mwezi huu kukagua kazi hii, na kila kitu kitajulikana hapo.”

Kampuni ya NAMIS ilipewa jukumu la kutekeleza mradi huo kwa kipindi cha miezi tisa ambapo mkataba wa utekezaji ulianza Desemba 10, 2019 na utakoma Septemba 9, 2020 kwa kukamilisha kazi zote za kusambaza umeme na kuunga wateja katika vijiji



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto), akifurahia jambo na Ally Zolila, mkazi wa kijiji cha Mhaga wilayani Kisarawe, kinachopitiwa na Mradi wa Usambazaji wa Umeme katika Vijiji vilivyo pembezoni mwa Miji (Peri Urban). Naibu Katibu Mkuu alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekezaji wa mradi husika, wilayani humo, Julai 11, 2020.

vyote 62 vilivyo pembezoni mwa miji (Peri Urban) katika maeneo ya Kisarawe mkoani Pwani na Ilala mkoani Dar es Salaam.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kampuni hiyo Mhandisi Thomas Uisso, alimhakikishia Naibu Katibu Mkuu kuwa atakamilisha kazi hiyo kwa wakati, kwa mujibu wa mkataba, licha ya kuwa nyuma ya muda, kwakuwa

miundombinu na vifaa vyote vinavyohitajika eneo la mradi vipo, na watakachofanya ni kuongeza nguvu kazi ili kazi hiyo ifanyike usiku na mchana na kwa haraka.

Aliwaomba wananchi waliopo katika maeneo yanayopitiwa na mradi huo kujiandaa kuunganishiwa umeme kwa kutandaza nyaya katika nyumba zao na kulipia gharama za

kufungiwa umeme huo ambayo ni shilingi 27,000 tu.

Wakati wa ziara ya Rais Dkt. John Magufuli Kisarawe, mkoani Pwani, mwishoni mwa Juni, 2020 aliigiza Kampuni hiyo ya NAMIS kuvuta nyaya katika nguzo zote ilizozisimika katika Wilaya hiyo.



Kamera ya Mwandishi wetu ilimulika kijana Amos Malima, Mkazi wa Kijiji cha Vilabwa aliyekuwa akijaza mafuta aina ya petroli katika chupa ndogo zilizoisha maji kutoka katika galoni kubwa lililoisha mafuta ya kupikia. Uwekaji wa mafuta ya petroli katika mazingira yasiyo salama ni hatari kwakuwa yanaweza kusababisha ajali ya moto. Tukio hilo lilinaswa wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, kukagua maendeleo ya utekezaji wa Mradi wa Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyo pembezoni mwa Miji (Peri Urban), Wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, Julai 11, 2020.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akitoa maagizo kwa Ujumbe alioambatana nao wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya Mradi wa kusambaza Umeme katika Vijiji vilivyo pembezoni mwa Miji (Peri Urban) Wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, Julai 11, 2020.

NAIBU WAZIRI MGALU AKAGUA UJENZI WA VITUO VYA KUPOZA UMEME

Hafsa Omar - Tabora

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Julai 8, 2020 alifanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi ya vituo vya kupoza umeme vilivyopo Katavi na Tabora.

Ziara hiyo ilihusisha ukaguzi wa Mradi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Ipole Tabora hadi Mpanda Katavi, ambapo alikagua kituo cha Inyonga kilichopo mkoani Katavi na kituo cha Ipole kilichopo mkoani Tabora.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya ukaguzi huo, Naibu Waziri alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu na kuzalisha umeme takribani megawati 28 za awali.

Aliwataka wakandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha mradi huo unakamilika

kwa wakati ili kufanikisha lengo la mikoa hiyo kuanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa.

"Mradi huu wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa katika Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa vipaumbele vyetu hivyo tutaendelea kuusimamia ili ukamilike kama ulivyopangwa," alisisitiza.

Pia, alikiri kufurahishwa na kupungua kwa gharama za ujenzi wa mradi ambao hapo awali ulikuwa ugharimu kiasi cha shilingi bilioni 135 lakini kwasasa utagarimu shilingi bilioni 70 tu.

Alilipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa usimamizi mzuri na kuwataka

watendaji wake kuendelea usimamizi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme katika mradi huo sanjari na kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo ili ukamilike kwa haraka.

Kwa upande wake, Meneja wa Mradi huo, Mhandisi Neema Mushi alisema, hadi sasa vituo vyote vipo katika hatua ya ujenzi ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2020.

Alisema, mradi huo utakapokamilika, utazalisha umeme kiasi cha megawati 28 za awali kwa matumizi ya viwanda na wananchi.

Awali, akiwa mkoani Katavi, Naibu Waziri aliwasha umeme katika kijiji cha Nsekwa kilichopo, Wilaya ya Mlele na kuwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi kwa sababu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu hivyo wakazi wa Katavi watapata umeme wa uhakika.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati) akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Katavi, wakikagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Inyonga, kilichopo Wilaya ya Mlele, Mkoani Katavi, Julai 8, 2020.



Mafundi wakindelea na ujenzi wa cha kituo cha kupoza umeme cha Inyonga, kilichopo Wilaya ya Mlele, Mkoani Katavi, Julai 8, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika kijiji cha Nsekwa, Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Julai 8, 2020. Kulia ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Katavi.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati) akikagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ipole, kilichopo Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora, Julai 8, 2020.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (alijekaa) akipewa baraka na kiongozi wa kimila wa kijiji cha Nsekwa, wakati alipokwenda kuwasha umeme kwenye kijiji hicho Julai 8, 2020.



Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), Adam Zuberi (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo, baada ya ziara yao kukagua ujenzi na ufungaji wa Midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika bandari ya Dar es Salaam, Julai 9, 2020.



Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), wakisikiliza maelezo ya ufanyaji kazi wa Midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika bandari ya Dar Es Salaam. Kamati hiyo ilikuwa katika ziara ya kukagua ujenzi na ufungaji wa midaki hiyo, Julai 9, 2020. Katikati ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi.

PSC YARIDHISHWA NA UFUNGAJI MIDAKI YA KISASA BANDARI YA DSM

**Zuena Msuya -
Dar es Salaam**

Kamati inayosimamia mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), imekiri kuridhishwa na kasi ya ufungaji wa Midaki, maarufu kama 'Scanner' katika Bandari ya Dar es Salaam, ilipofanya ziara Julai 9, 2020.

Midaki hiyo inayoongoza kwa ukubwa na ya kisasa Afrika, inatumia mionzi kukagua mizigo katika Bandari hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati husika, Mhandisi Zena Said ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kaimu Mwenyekiti Adam Zuberi, alisema ujenzi wa jengo la Midaki hiyo umekamilika kwa asilimia 99 huku usimikaji na ufungaji wa vifaa ukiwa umefikia asilimia 51.

Zuberi ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi, alieleza zaidi kuwa, kazi hiyo ya usimikaji

na ufungaji wa vifaa inatarajiwa kukamilika Septemba, 2020 kwa gharama ya takribani Dola za Marekani milioni tano.

"Midaki hiyo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kukagua magari makubwa ya mizigo yapatayo 200 kwa saa, hivyo itarahisisha utendaji kazi katika bandari ya Dar es Salaam na kuwahudumia wateja kwa haraka zaidi," alifafanua.

Aidha, alieleza kuwa, Midaki husika itakuwa na uwezo wa kubaini aina mbalimbali za mizigo inayoingia na kutoka nje ya nchi kupitia bandari hiyo hivyo kuondoa udanganyifu uliokuwa unafanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, waliokuwa wakipitisha bidhaa tofauti na zile zilizoelzwa katika nyaraka husika.

Alisema kuwa, midaki hiyo itaongeza kwa kiasi kikubwa kasi ya ukusanyaji mapato ya serikali kwa kuwa itakuwa na uwezo mkubwa wa kubaini na kukagua kila kitu kilichomo

katika shehena ya mzigo ili ilipiwe kodi stahiki.

"Midaki hii ni muhimu sana kwa Taifa letu kwani itarahisisha ukusanyaji wa mapato, kubaini kilichobebwa ndani ya gari, na kusafirisha mizigo kwa haraka zaidi," alisema Zuberi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio, aliwahakikishia watanzania kuwa ana imani midaki hiyo itakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa kwa kuwa asilimia kubwa ya utekelezaji wa mradi huo imekamilika.

Vilevile alieleza kuwa, midaki hiyo mpya itakayotumia teknolojia ya kisasa, itaboresha ukusanyaji wa mapato serikalini na kurahisisha utendaji kazi katika kukagua mizigo mingi itakayokuwa ikipita kwa wakati mmoja na kwa haraka zaidi.

Alisema kuwa mionzi iliyopo katika midaki hiyo, haitakuwa na madhara

kwa watumiaji kwa sababu wakandarasi wanaoijenga wamezingatia sheria na taratibu za afya na usalama sehemu za kazi.

Naye Meneja wa mradi huo, Asjadi Mrutu alisema kuwa, mbali na ujenzi wa midaki hiyo, pia mifumo ya utendaji kazi katika bandari zote nchini na katika viwanja vya ndege itaboreshwa, ikiwa ni pamoja na kuondoa shehena za mizigo zilizo mipakani.

Alibainisha kuwa, wanufaika wa mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kushirikiana na Serikali ni Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Wengine ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Baraza la Uwezesaji la Taifa (NEEC), Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Mafuta Zanzibar (ZURA) pamoja na Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato Zanzibar (TRA-ZANZIBAR.)

Mradi huo unasimamiwa na kutekelezwa na Wizara ya Nishati kupitia TPDC.



Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), wakikagua maendeleo ya ujenzi na ufungaji Midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika bandari ya Dar es Salaam, Julai 9, 2020.

Msimamizi wa ujenzi na ufungaji wa midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam, Mhandisi Joseph Raymond (kulia), akitoa maelezo ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo kwa Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa Mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), walipofanya ziara kukagua ujenzi na ufungaji wa midaki hiyo Julai 9, 2020.



Midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), kukagua ujenzi na ufungaji wa midaki hiyo, Julai 9, 2020.

Jengo la kuendeshea mitambo na udhibiti Midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa Mradi wa uboreshaji wa Taasisi za usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC) Julai 9, 2020.



Mwonekano wa Jengo la midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam, lililokamilika kwa zaidi ya asimilia 90. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC) Julai 9, 2020.

Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa mradi wa uboreshaji wa Taasisi za Usimamizi wa Rasilimali Asilia na Ukusanyaji wa Mapato (PSC), wakiwa katika kikao cha mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020 kabla ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi na ufungaji wa midaki (Scanner) kubwa na ya kisasa Afrika ya kukagua mizigo inayopita katika bandari ya Dar es Salaam, Julai 9, 2020.

TUNAO UMEME WA UHAKIKA KUENDESHA TRENI YA MWENDOKASI - SERIKALI

Veronica Simba

Serikali imewataka Watanzania kuondoa hofu kuhusu upatikanaji umeme wa uhakika utakaowezesha matumizi ya Treni ya kisasa ya mwendokasi, inayoendelea kujengwa nchini.

Akizungumza mkoani Morogoro, Juni 29 mwaka huu, wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi la ujenzi wa mahandaki itakamopita reli hiyo, Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani alisema serikali imejipanga kutumia vyanzo vikubwa vitatu vya umeme, vilivyopo nchini katika kukidhi mahitaji husika.

“Baadhi ya watu wanaweza kujiuliza hivi tutaweza kweli kutembeza treni ya



Mwonekano wa sehemu ya miundombinu ya Treni ya kisasa ya mwendokasi itakayotumia umeme (SGR), kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa kwanza-kulia) pamoja na viongozi wengine mbalimbali, wakishuhudia Rais John Magufuli, akiweka jiwe la msingi ujenzi wa mahandaki itakamopita Treni ya kisasa ya mwendokasi inayotumia umeme (SGR), Juni 29, 2020.

kisasa ya mwendokasi kwa umeme! Naomba niwaondolee wasiwasi Watanzania maana tunavyo vyanzo vikubwa vitatu vitakavyunganisha umeme katika Treni hii.”

Dkt Kalemani alivitaja vyanzo hivyo kuwa ni pamoja na umeme wa gesi unaozalishwa katika mitambo ya Kinyerezi jijini Dar es Salaam, umeme unaozalishwa Mtera na Kidatu pamoja na umeme utakaozalishwa kupitia Mradi mkubwa wa Julius Nyerere, ulioko Rufiji mkoani Pwani.

“Kwahiyo Mheshimiwa Rais na Watanzania wote, Treni hii haitasimama, eti kwa kukosa umeme,” alisisitiza.

Akifafanua zaidi namna



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli (wa saba kutoka kulia) akikata utepe kabla ya kuweka rasmi jilwe la msingi la ujenzi wa mahandaki itakamopita Treni ya kisasa ya mwendokasi inayotumia umeme (SGR), Juni 29, 2020. Wa nne kutoka kulia ni Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani.

TUNAO UMEME WA UHAKIKA KUENDESHA TRENI YA MWENDOKASI - SERIKALI

INATOKA UK.

17

Serikali ilivyojipanga katika kufanikisha Mradi huo, Waziri alisema kuwa mabehewa ya Treni hiyo yatafungwa mitambo inayoweza kuhifadhi umeme kwa muda wa nusu saa hadi saa nzima, kwa matumizi ya dharura hususan ikitokea umeme umekatika.

Alimpongeza Rais John Magufuli kwa uthubutu wa kutekeleza Mradi huo

akisema Tanzania ni ya kwanza katika nchi za Afrika Mashariki kuwa na Treni ya aina hiyo na itakuwa ya nne Afrika ikizifuatia nchi za Afrika Kusini, Morocco na Nigeria.

Katika hatua nyingine, Waziri Kalemani pia alitumia fursa hiyo kuwapa uhakika wananchi wa Kilosa mkoani Morogoro kuwa serikali itafikisha umeme katika vijiji vyao vyote vilivyosalia.

"Kilosa ina vijiji 138. Vijiji 91 tayari vina umeme na 37 ndivyo vimebaki.

Kuanzia mwezi ujao, tunaanza kusambaza umeme katika vijiji vyote 671 vya Mkoa wa Morogoro pamoja na vitongoji vyake."

Akizungumza katika hafla hiyo, Mgeni Rasmi, Rais Magufuli alisema pamoja na Serikali yake kusambaza kwa kasi umeme vijijini, pia imejiwekea mkakati kuhakikisha gharama za nishati hiyo zinaendelea kushuka ili kuwawezesha Watanzania wote kuutumia.

"Mradi wa umeme wa

Julius Nyerere utakapoanza kuzalisha umeme, bei ya nishati hiyo itashuka zaidi na viwanda vyetu vitapata umeme wa kutosha, vijana wetu watapata ajira na uchumi wetu utapanda."

Aidha, Rais Magufuli alisema juhudi na maarifa ambayo Watanzania wameamua kusimamia kwa pamoja, ndivyo vimeendelea kuwezesha maendeleo katika sekta mbalimbali nchini ikiwemo umeme, ambao alisema hadi sasa umefika katika vijiji zaidi ya 9,000.

MGALU AFANYA ZIARA JNHPP



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye shati la pinki) na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manyanya, wakikagua ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji wakiwa wameambatana na wadau mbalimbali, Julai 2, 2020.

Hafsa Omar - Pwani

Naiibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Julai 2, 2020 amefanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji.

Katika ziara yake hiyo, aliambatana na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati.

Akizungumza na waandishi wa habari mara

baada ya kumaliza ukaguzi wa mradi huo, alisema ameridhishwa na hatua iliyofikiwa katika mradi huo na kwamba inaleta matumani ya kumalizika kwa wakati kwa mradi huo.

“Sisi Wizara ya Nishati tutaendelea kusimamia Mradi huu kikamilifu tena kwa ari kubwa, ili tutimize lengo la Rais wetu la kuukamilisha kwa wakati kama ilivyopangwa. Niwapongeze sana wakandarasi kwa kufanya kazi nzuri mpaka sasa,” alisema Mgalu.

Alisema, Mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kuzalisha umeme wa megawati

2,115 na kuongeza kuwa, utakuwa mkombozi kwa wenye viwanda, wafanyabiashara pamoja na wananchi wa kawaida nchini kwa sababu utakuwa mwingi na wenye bei nafuu.

Alitaja moja ya faida kubwa za Mradi huo ni kutoa ajira, ambapo mpaka sasa, zaidi ya Watanzania 3,000 wameajiriwa katika mradi huo ambao unatarajia kutoa ajira zaidi ya 6,000.

Akieleza zaidi faida za Mradi huo alisema ni pamoja na kutoa fursa kwa Kampuni za wazawa ambazo zinazuza bidhaa zao kwenye Mradi husika.

Katika hatua

nyingine, alizitaka Kampuni zilizopewa kazi mbalimbali katika Mradi huo kufanya kazi kwa bidii kwa kushirikiana na Mkandarasi wake ili kukamilisha Mradi kwa wakati.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manyanya, alisema Wizara yake ni moja ya wadau wakuu wa Mradi huo kwani umeme utakaozalishwa utawanufaisha wazalishaji viwandani pamoja na

INAENDELEA UK. 20



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye shati la pinki) na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manyanya, wakikagua ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji wakiwa wameambatana na wadau mbalimbali, Julai 2, 2020.

MGALU AFANYA ZIARA JNHPP

INAENDELEA UK. 19

wafanyabiashara nchini.

Aidha, alitoa wito kwa Watanzania kuwekeza katika viwanda na biashara mbalimbali kwani umeme wa uhakika unatarajiwa kupatikana mara baada ya kukamilika kwa Mradi husika.

Alieleza kuwa, Mradi huo ukikamilika, utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa viwanda nchini kutokana na upatikanaji umeme wa uhakika na wenye gharama nafuu hivyo wafanyabiashara wataendesha biashara zao kwa faida kubwa.

Aliongeza kuwa, amefurahishwa na mahusiano mazuri kati ya Mkandarasi wa Mradi husika pamoja na Watanzania wanaofanya kazi katika Mradi huo.

Aliwataka vijana ambao wanapata ujuzi kwenye Mradi huo, kutumia ujuzi watakaoupata kuanzisha miradi midogo midogo ya kuzalisha umeme.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani), Julai 2, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji, Julai 2, 2020.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaotekelezwa kwenye mto Rufiji, Julai 2, 2020 akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani).

ZIARA YA NAIBU KATIBU MKUU MASANJA JNHPP

Zuena Msuya - Pwani

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja ametembelea na kukagua mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP).

Mhandisi Masanja

alifanya ziara hiyo Julai 17, 2020 ambapo pamoja na mambo mengine alizungumza na wasimamizi na waratibu wa utekezaji wa ujenzi wa Mradi huo kujua maendeleo yake.

Pia, alitembelea maeneo mbalimbali ili kuona maendeleo ya ujenzi wa Mradi huo ambapo alikiri kuridhishwa na maendeleo yake.



Mwonekano wa mahandaki mawili kati ya matatu yatakayotumika kama njia ya kupeleka maji katika mashine za Mradi wa kufua umeme wa maji kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JHPP). Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi huo, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (wa pili kulia) akipewa maelezo ya ujenzi wa handaki la kupeleka maji katika mashine za Mradi wa kufua umeme wa maji kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi huo, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (wa pili kulia), akikagua kazi inayofanywa na mafundi (hawapo pichani), wanaoendelea na kazi ya ujenzi wa handaki la kuchepusha maji katika Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wake, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (wa pili kulia), akikagua kazi inayofanywa na mafundi (hawapo pichani), wanaoendelea na kazi ya ujenzi wa handaki la kuchepusha maji katika Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wake, Julai 17, 2020.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa handaki la kuchepusha maji katika Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP). Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (kushoto), akizungumza na wasimamizi wa ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi huo, Julai 17, 2020.



Wasimamizi wa utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (hayupo pichani) alipokuwa akuzungumza nao wakati alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi huo, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja (wa pili kulia) akipewa maelezo ya ujenzi wa kuta/kingo za maji katika Mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi huo, Julai 17, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Nishati akagua Mradi wa umeme unaotekelezwa na wazalishaji binafsi

Zuena Msuya - Njombe

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja amesema kuwa Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wazalishaji binafsi wa umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mito iliyopo nchini. Mhandisi Masanja alisema hayo Julai 25, 2020 alipofanya ziara ya kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji wa Mapembasi uliopo katika Kijiji cha Itanduka, Kata ya Ihanga, Wilaya na Mkoa wa Njombe unaotekelezwa na Kanisa Katoliki.

Aidha, alisema kuwa jukumu la Serikali kupitia Wizara ya Nishati ni kutunga Sera na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika Sekta ya Nishati.

“Kwa muktadha huo, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake, itaendelea kusimamia sheria, taratibu na kanuni za uwekezaji katika sekta ya nishati ili kuendelea kuvutia wawekezaji nchini.”

Baada ya kukagua

miundombinu katika eneo la Mradi, Naibu Katibu Mkuu alitoa maelekezo kuwa ifanyike tathmini kwa kuunda Timu ya wataalamu kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na Mradi wa Mapembasi.

Sambamba na hilo, aliagiza kufanyike tathmini ya gharama za miundombinu iliyopo pamoja na mabesho yatakayohitajika, huku Wizara ikiendelea na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa miradi yote inayotekelezwa na wazalishaji wadogo wa umeme ili kubaini changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Akifafanua zaidi, alisema kuwa, umeme unaozalishwa kwa kutumia maporomoko ya maji ni umeme wa gharama nafuu zaidi kulinganisha na vyanzo vingine vya kuzalisha umeme.

“Tanzania tumejaaliwa kuwa na mito mingi inayotumiwa kama vyanzo vya kuzalisha umeme. Serikali iko bega kwa bega na wazalishaji binafsi wa umeme ili kuhakikisha umeme unakuwa mwingi,



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) na Ujumbe wake, wakisisikiliza maelezo kutoka kwa Padri Rortunatus Mwinuka (kushoto) kuhusu Mradi unaotekelezwa na Kanisa Katoliki wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji wa Mapembasi ulioko wilayani Njombe, Mkoa wa Njombe, Julai 25, 2020.

wa kutosha, na wa uhakika ili kila mtanzania aweze kutumia nishati hiyo kwa gharama nafuu wakati wote kwa kujiletea maendeleo yake binafsi na taifa kwa ujumla,” alisema Mhandisi Masanja.

Alisema kuwa Vijiji na vitongoji vinavyopitiwa na miundombinu ya umeme kuelekea eneo la mradi vipatiwe umeme kupitia TANESCO.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mradi wa Mapembasi, Padri Fortunatus Mwinuka alieleza kuwa, kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme wa msongo wa Kilovoti 33, yenye urefu wa kilometa 23 na kusimika transfomana katika kata ya Ihanga, ambapo zaidi ya shilingi milioni 900 (922,782,139) zilitolewa na Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini kwa ajili ya ujenzi wa

miundombinu hiyo.

Mradi huo wa Mapembasi unatarajiwa kuzalisha umeme wa Megawati 10 katika Mkoa wa Njombe. Ulianzishwa Mwaka 2009 kwa ushirikiano wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Njombe na Wadau wa Maendeleo wa Mkoa huo.

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Meneja wa TANESCO mkoani Njombe, Mhandisi Rukia Mpako pamoja na Meneja Mwandamizi wa Shirika hilo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Salome Mkondola.

Wengine ni Mhandisi Eric Rugabera kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) pamoja na Mhandisi Cosmas Kigulli wa Wizara ya Nishati.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) na Ujumbe wake, wakiangalia Jiwe la Msingi la Mradi unaotekelezwa na Kanisa Katoliki wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji wa Mapembasi ulioko wilayani Njombe, Mkoa wa Njombe, akiwa katika ziara ya kazi, Julai 25, 2020. Jiwe hilo liliwekwa mwaka 2013 na Rais Mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete.



Padri Aurelian Mwinuka (katikati) akionesha miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme (haipo pichani) kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga (kushoto), wakati wa ziara ya kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji, Mapembasi, ulioko wilayani Njombe, Mkoa wa Njombe, Julai 25, 2020.



Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mkoa wa Njombe, Mhandisi Rukia Mpako (kulia) na Meneja wa Shirika hilo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Salome Mkondola, wakijadiliana jambo wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (hayupo pichani) kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji unaotekelezwa wilayani humo, Julai 25, 2020.



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga (wa tano- kushoto), akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) na Ujumbe aliombatana nao katika ziara ya kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji, Mapembasi, ulioko wilayani Njombe, Mkoa wa Njombe, Julai 25, 2020.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa pili-kushoto), akiwa nje ya Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Njombe, alipofanya ziara ya kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji, Mapembasi, ulioko wilayani Njombe, Mkoa wa Njombe, Julai 25, 2020. Wengine (kutoka kushoto) ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Njombe, Mhandisi Rukia Mpako, Mhandisi Cosmas Kigulli kutoka Wizara ya Nishati na Mhandisi Eric Rugabera kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa tano-kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na viongozi pamoja na wataalamu kutoka wizarani, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) baada ya ziara yake kukagua Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuji, Mapembasi unaotekelezwa na Kanisa Katoliki wilayani Njombe Julai 25, 2020.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

-  www.nishati.go.tz
-  [Wizara ya Nishati](#)
-  [@Nishati2017](#)
-  [wizara_ya_nishati_tanzania](#)
-  [Wizara ya Nishati](#)